**Journal of Kiswahili and Other African Languages**
Vol. 2 No. 2 (2024): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/jkal.v2i2.687


# Uhakiki wa Itikadi Zilizofumbatwa Kijazanda kwenye Nyimbo za Kiasili za Kikamba

**Elizabeth K. Mue, Magdaline N. Wafula & Robert Oduori**
*Moi University, Kenya*

**Uwasilishaji wa Makala**
*Pokelewa: 2024-04-22*
*Rekebishwa: 2024-08-02*
*Kubalika: 2024-08-21*
*Chapishwa: 2024-08-29*

***Maneno Muhimu***
Asilia
Itikadi
Jazanda
Nyimbo

**Jinsi ya Kurejelea Makala:**
Mue, E. K., Wafula, M. N. & Oduori, R. (2024). Uamilifu wa Jazanda Kwenye Nyimbo za Kiasili za Kikamba. *Journal of Kiswahili and Other African Languages*, 2(2), 34-43.

*Copyright © 2024*
CC BY NC SA

**Ikisiri**
Makala haya yanachunguza itikadi zilizofumbatwa kijazanda katika nyimbo za kiasili za Kikamba. Lengo kuu la makala ni kuhakiki itikadi za Wakamba zinazofumbatwa kijazanda kwenye nyimbo teule. Uchunguzi huu ni wa kithamano. Mbinu ya kimaelezo ilitumika katika ukusanyaji na uchanganuzi wa data. Data ya kimsingi ilitokana na nyimbo nane za kiasili za Kikamba zinazosheheni jazanda. Nyimbo zenyewe zilikusanywa kutoka Tume ya *Permanent Presidential Music Commission* nchini Kenya. Uteuzi huo ulifanyika kimaksudi kwa maana utafiti ulilenga kuhakiki itikadi zinazofumbatwa kijazanda kwenye nyimbo teule. Data ya uchunguzi huu imechanganuliwa na maelezo kutolewa kulingana na lengo la utafiti na mihimili ya kinadharia. Utafiti umeongozwa na Nadharia ya Jazanda Dhanifu na ile ya Itikadi. Kimsingi, huu ni utafiti wa maktabani kwa kuwa data muhimu zilitokana na rekodi zilizowekwa. Matokeo ya utafiti yalibainisha kuwa nyimbo za kiasili za Kikamba huwasilisha itikadi za Wakamba zilizofumbatwa kijazanda. Itikadi zenyewe zimejikita katika masuala kama vile tohara, kazi, ndoa na mapenzi, ubikira, utamaduni, malezi na mauti. Matokeo ya utafiti huu yanakuza maarifa kuhusiana na dhima ya kipera cha nyimbo katika fasihi simulizi za Kiafrika. Makala haya yanapendekeza kwamba ufasiri wa jazanda kwa mujibu wa nadharia ya Udenguzi ufanywe ili kubaini fasiri mbalimbali kwa mujibu wa hadhira.

## Utangulizi

Fasihi simulizi ya Wakamba huhusisha vipera mbalimbali nyimbo za kiasili zikiwemo. Nyimbo za kiasili ni maarufu na ni sehemu ya takriban kila shughuli na hafla za jamii ya Wakamba. Kupitia nyimbo hizi, itikadi ya Wakamba huwasilishwa kwa hadhira. Hata hivyo, itikadi hii aghalabu hufumbatwa kijazanda. Makala haya yanahakiki itikadi za Wakamba zinazofumbatwa kijazanda kwenye nyimbo teule za kiasili.

Kulingana na Vincent (1992), dhana ya itikadi ni changamano kwa vile inaweza kufasiliwa kwa namna mbalimbali. Wataalam mbalimbali wameifafanua dhana hii kwa namna tofauti. Hawa ni kama vile Gramsci (1985), Eagleton (2007), Althusser (1984), Van Djik (1998) na Gianetti (2013). Utafiti huu unaichukulia itikadi kuwa mkusanyiko wa mawazo, imani, maadili, mitazamo na tabia ambazo kwake, wanajamii hujenga maana ya ulimwengu wao na mambo yaliyomo. Mohamed (1995) anaeleza kwamba itikadi ya mtunzi hutegemea mambo kama vile, mahali alikozaliwa na mazingira alimokulia, imani au dini yake na nafasi yake kiuchumi. Kwa hivyo, mtunzi wa kazi za kifasihi, akiwa sehemu ya jamii, huathirika sana na itikadi za jamii yake na ambazo bila shaka hujitokeza katika kazi zake za kifasihi. Hii ndiyo sababu Van Dijk (1998) anaeleza kwamba itikadi huwa za kijamii kwa vile

huzalishwa na kudumishwa na jamii nzima. Kwa hivyo, mtunzi wa nyimbo za kiasili za Kikamba hana budi kuzingatia itikadi za jamii yake kwa vile hadhira inayolengwa ni ya Wakamba. Khan (2021) akiangazia uhusiano ulioko baina ya fasihi na jamii anathibitisha kuwa fasihi ni kioo kinachoakisi maisha ya jamii japo akisiko hilo hutegemea mahali kilikowekwa kioo hicho. Ni kwa msingi huu ndipo tunadai kuwa mtunzi wa kazi za fasihi hutumia fasihi kama jukwaa la kuielimisha jamii kuhusiana na itikadi maalum. Mahitimisho ya makala haya yametokana na uchunguzi wa nyimbo za kiasili za Kikamba nane. Nyimbo zenyewe ni: *Sisya Wone*, *Kaveti Kaanu*, *Uka Usuvie Utwae*, *Sikala*, *Kithio kya Mukamba*, *Kyathi noVala*, *Inyaa Mwana na Ithea Mwana* pamoja na *Kikw'u ni Musyimi*. Nyimbo hizi za kiasili huimbwa kwenye hafla mbalimbali kama vile za tohara, kazi, ndoa na arusi, sherehe za kuzaliwa kwa watoto na mazishi.

**Mbinu za Ukusanyaji na Uwasilishaji wa Data**

Makala haya yanatokana na utafiti wa nyimbo za kiasili za Kikamba zinazosheheni jazanda mbalimbali. Nyimbo hizi zilisampuliwa kimakusudi ambapo nyimbo zinazoimbwa katika hafla mbalimbali za kijamii miongoni mwa Wakamba ziliteuliwa. Utafiti ulichukua mkabala wa kithamanio ambapo uchanganuzi wa data na maelezo yake ulizingatia mihimili ya kinadharia iliyoongoza utafiti huu. Nyimbo za kiasili za Kikamba 100 zilikusanywa kutoka tume ya *Permanent Presidential Music Commission* nchini Kenya na kuhifadhiwa katika diski. Baada ya kupata idadi aliyolenga, mtafiti alizisikiliza kwa makini na kuteua nyimbo ambazo zinawasilisha itikadi kijazanda na kuzinakili katika daftari. Kwa mujibu wa makala haya, nyimbo 8 pekee ndizo ziliteuliwa na kuchanganuliwa. Data iliyokusanywa ilitafsiriwa, ikapangwa na kuchanganuliwa kulingana na lengo la utafiti. Uchanganuzi na ufasiri wa data umeongozwa na lengo la utafiti pamoja na mihimili ya nadharia za utafiti. Lengo lenyewe ni kuhakiki itikadi za Wakamba zinazofumbatwa kijazanda kwenye nyimbo teule. Baada ya uchanganuzi na ufasiri wa data, upangaji na uwasilishaji wa matokeo umefanywa kwa njia ya kimaelezo.

**Msingi wa Kinadharia**

Uchunguzi huu umeongozwa na nadharia Nadharia ya Itikadi kwa mujibu wa Van Djik (1998) na Nadharia ya Jazanda Dhanifu ilivyofafanuliwa na Lakoff na Johnson (1993).

**Nadharia ya Itikadi**

Kulingana na Van Djik (1998, itikadi ni maumbo ya kimsingi ya utambuzi wa kijamii. Maumbo yenyewe huundwa kwa maadili teule ya kijamii na kitamaduni. Kwa hivyo, maadili yoyote hupangwa kwa umbo na muundo wa kiitikadi unaowakilisha ufafanuzi, uelewa na ufasiri wa kikundi maalum cha jamii. Hii inamaanisha kuwa, kila jamii ina maumbo maalum ambayo yanasheheni itikadi zake. Kwa hivyo, mtafiti wa fasihi hana budi kuchunguza uamilifu wa kiitikadi katika utanzu wa fasihi unaohusika. Katika makala haya tumeangazia mihimili ifuatayo ya nadharia hii: maadili, miundo ya itikadi, mielekeo, maumbo, maumbo ya muktadha, tambuzi nyinginezo za kibinafsi na miundo yenye upendeleo au maumbo ya kiitikadi.

***Maadili***

Mhimili wa maadili unashikilia kwamba itikadi ni mifumo ya utambuzi wa kijamii ambayo inaweza kutathminiwa. Itikadi huweka msingi wa maamuzi kuhusu kilicho kizuri au kibaya na pia hutoa mwongozo wa kimsingi wa mtazamo na maingiliano ya kijamii. Vijenzi vikuu vya itikadi ni maadili. Kwa mfano, katika wimbo *Kaveti kaanu* (Kijike kizembe), mwimbaji anakejeli uzembe na kwa hivyo anapitisha maadili ya bidii kazini.

***Miundo ya Itikadi***

Mhimili wa miundo ya itikadi unadai kwamba itikadi huwa zimejipanga kwa namna mbalimbali. Kwa hivyo miundo maalum hupambanua makundi au aina maalum ya itikadi. Kwa mfano, katika

wimbo *Uka Usuvie Utwae* (Njoo Uitunze Ndoa) itikadi iliyofichwa hapa ni kwamba jinsia ya kike inaelekea kutwikwa jukumu kubwa la kuitunza ndoa ikilinganishwa na jinsia ya kiume. Kwa hivyo, wimbo huu unapoimbiwa wanandoa katika Karne ya 21 huenda ukafasiriwa vinginevyo hasa na wale wanashikilia mkabala wa usawa wa kijinsia katika majukumu ya wanandoa.

***Mielekeo***

Mhimili wa mielekeo unadai kwamba dhima moja kuu ya kiutambuzi-kijamii ya itikadi ni kupanga makundi maalum ya maoni yanayohusiana na masuala ya kijamii. Nyimbo za kiasili za Kikamba hupitisha itikadi anuai. Ipo mielekeo maalum inayohusiana na itikadi hizo. Mielekeo hiyo hushikiliwa na tabaka maalum katika jamii. Tabaka hilo huchukulia maoni yao ndiyo sahihi na kwa hivyo hujitahidi kushinikiza wanajamii wote kuchukua mwelekeo wao. Hali hii inajitokeza katika wimbo *Sikala* (Sigara). Neno sigara limetumika kijazanda kurejelea ngono. Wimbo huu unawasilisha mwelekeo wa kiitikadi kuhusu ubikira kwamba vijana Wakamba hasa wa kike hawana budi kusalia mabikira hadi pale wanapopata ndoa.

***Maumbo***

Kwa mujibu wa mhimili huu, maumbo yanarejelea uwakilishaji wa kiakili wa tajriba za kibinafsi kuhusu shughuli, matukio au hali maalum. Maumbo hayo yanaweza kurejelea matukio yaliyopita, yaliyopo na yajayo. Kwa hivyo kila jamii huwa na maumbo maalum ambayo hutumiwa kupambanua maarifa na tajiriba zao mbalimbali.

Utafiti huu umetambua kwamba waimbaji wa nyimbo za kiasili za Kikamba wanashiriki maarifa maalum ya kimsingi kuhusiana na utamaduni wa jamii ya Wakamba. Hii ndiyo sababu unapata nyimbo mbili tofauti zinaweza kuwasilisha itikadi moja. Kwa mfano, wimbo *Kyathi no Vala* (Miadi ni ile ile) na *Inyaa Mwana na Ithea Mwana* (Mama na Baba Mtoto) zinawasilisha itikadi kuhusu malezi. Nyimbo hizi zinapitisha ujumbe kwamba kila mwanajamii ana jukumu lake katika malezi ya watoto ambao ni mali ya jamii.

***Maumbo ya Muktadha***

Mhimili wa maumbo ya muktadha unashikilia kwamba umbo la muktadha hutekeleza wajibu muhimu katika matini na mawasiliano. Umbo la muktadha ni uwakilishaji wa matukio, hali na watendaji. Kwa mfano, uelewekaji wa nyimbo za kiasili za Kikamba hutegemea muktadha wa uwasilishaji. Mhimili huu umetuongoza kutambua kuwa nyimbo za kiasili za Kikamba huwasilishwa kwenye hafla rasmi au zisizokuwa rasmi. Kwa mfano, nyiso za Kikamba huimbwa kwenye hafla rasmi huku bembezi za Kikamba zikiwasilishwa kwenye hafla zisizokuwa rasmi. Kwa hivyo, mhimili huu ni muhimu katika kupambanua shughuli za kijamii na thamani yazo kijamii.

***Tambuzi Nyinginezo za Kibinafsi***

Mhimili wa tambuzi za kibinafsi unasisitiza umuhimu wa maarifa ya kimsingi katika ufafanuzi wa itikadi. Maarifa yenyewe hutokana na tajriba zetu binafsi kutegemea hasa wakati na mahali wanakopatikana wanajamii. Maarifa haya ya kimsingi hudhihirika kupitia maoni ya mtu binafsi. Kama mzungumzaji mzaliwa wa lugha ya Kikamba, mtafiti alitumia utambuzi wake wa kibinafsi kutokana na tajiriba yake kutoa fasiri ya jazanda na itikadi zilizofumbatwa na jazanda mahsusi.

***Miundo yenye Upendeleo***

Mhimili wa miundo yenye upendeleo unadai kwamba maoni ya kibinafsi pamoja na mielekeo ya kiitikadi inaweza kuathiri uundaji wa maumbo ya muktadha na matukio. Ni kupitia maumbo ya kiitikadi ambapo matini zenyewe zinaweza kutambuliwa au kufasiriwa kuwa itikadi. Mhimili huu ni muhimu kwa vile unathibitisha kuwa matini maalum inaweza kubeba au kughubika itikadi maalum.

Ni kwa msingi huu ndipo nyimbo za kiasili za Kikamba zinaaminika kupitisha itikadi mbalimbali. Kwa mfano, wimbo *Kwa Sisya Wone* (Angalia Uone) unapitisha itikadi kuhusu tohara.

**Nadharia ya Jazanda Dhanifu kwa mujibu wa Lakoff na Johnson (1993)**
Nadharia ya Jazanda dhanifu inajihusisha na ufasiri wa jazanda. Nadharia hii imefafanuliwa na wataalam mbalimbali ila kwa mujibu wa utafiti huu, mkabala wa Lakoff na Johnson (1993) ndio umezingatiwa. Lakoff na Johnson wanashikilia kwamba ufasiri wa jazanda unahusisha kufafanua uwanja dhanifu lengwa (B) kwa kurejelea uwanja dhanifu asilia (A). Yaani, dhana moja inafafanuliwa kwa misingi ya dhana nyingine. Nadharia ya Jazanda dhanifu ina mihimili mitatu mikuu ambayo inafaa kuzingatiwa katika ufasiri wa jazanda. Mihimili hii ni ukawaida wa jazanda, umbo dhanifu la jazanda na uhusishaji wa jazanda na tajriba halisi za wazungumzaji wa lugha katika mazingira husika. Mihimili hii ilitumika kuzifafanua jazanda zilizotumika katika nyimbo za kiasili za Kikamba ifuatavyo:

**i). *Ukawaida wa Jazanda***
Mhimili huu unashikilia kwamba jazanda hutumika kwa njia mbalimbali ambapo matumizi yake huzoeleka na watumiaji wa lugha inayohusika. Kwa hivyo, uzoefu wa maelezo ya kijazanda huimarisha maana za kimsingi katika akili za wazungumzaji wa lugha inayohusika. Kwa mfano, katika wimbo *Sikala* (Sigara), neno sigara limezoeleka kutumika kijazanda na Wakamba kurejelea ngono.

**ii). *Umbo Dhanifu la Jazanda***
Mhimili huu unashikilia kwamba jazanda ni tukio la lugha linalotumia dhana ili kuwasilisha dhana nyingine. Katika kuzifasiri jazanda, mfasiri anahamisha sifa za uwanja asilia (A) anaoufahamu, hadi katika uwanja lengwa (B) asioufahamu, ili kuelewa maana iliyokusudiwa. Mfano upo katika wimbo *Kikw'u ni Musyimi ute tei* (Kifo ni Mnyang'anyi asiye na huruma). Dhana ya *mwindaji asiye na huruma* limetumika kijazanda kurejelea *kifo*. Sifa za mwindaji asiye na huruma zinahamishwa kwa kifo ambapo maana iliyokusudiwa inafahamika. Jazanda hii inawasilisha itikadi kuhusu mauti kwamba huwanyang'anya watu wapendwa wao bila huruma.

**iii*). Uhusishaji wa Jazanda na Tajriba Halisi za Wazungumzaji wa Lugha katika Mazingira Husika***
Mhimili huu unaeleza kwamba ufasiri wa jazanda unahusisha kuelewa uzoefu halisi wa mtumiaji wa lugha. Uundaji, ufasiri na uelewekaji wa jazanda huhusisha mchakato wa kiutambuzi pamoja na uhamishaji wa maana kwa mujibu wa maarifa ya kimsingi yanayohusiana na mazingira yake. Mfano ni kupitia kwa wimbo *Kwa Sisya Wone* (Angalia Uone) ambapo neno *mbilano* (kazi**)** limetumika kijazanda kuwasilisha dhana ya kujamiana (ngono). Maarifa ya kimsingi kuhusiana na kazi yanaiwezesha akili ya msikilizaji kutambua dhana lengwa ambayo ni kujamiana. Itikadi inayowasilishwa hapa ni kwamba ngono ni shughuli muhimu kwa wanandoa. Kupitia kwa shughuli ya kujamiana jamii huendelezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

**Matokeo ya Utafiti**
Matokeo ya tafiti yalibainisha kuwa, katika jamii ya Wakamba, zipo itikadi za aina mbalimbali na ambazo hupitishwa kijazanda kwenye nyimbo zao za kiasili. Itikadi zenyewe zinahusu tohara, kazi, ndoa na mapenzi, ubikira, utamaduni, malezi na mauti miongoni mwa nyingine.

**Itikadi kuhusu Tohara**
Kwa mujibu wa TUKI (2013), tohara ni upasuaji mdogo wa kukata au kuondoa govi, yaani ngozi inayofunika ncha ya uume. Kwa mujibu wa utamaduni wa Wakamba, tohara ni kivukio cha kutoka utotoni hadi utu uzima. Itikadi ya tohara hudhihirika katika nyiso za Kikamba ambazo huimbwa katika hafla za tohara. Nyimbo hizi hubeba mafunzo mbalimbali kwa watahiriwa. Kwa mfano, wimbo

*Kwa Sisya Wone* (Angalia Uone) unapitisha itikadi kuhusu tohara kijazanda. Tazama mishororo ifuatayo:

Mwaiki: *Muti uu ni mumu. Muti uu ni mumu. Umite nza na nthini nomwiu. Ninguutila!*

Mwaikwa: *Ekai ukia ta matila ma kiimani matesi mbilano*
Tafsiri:
*Ngariba: Mti huu umekauka. Mti huu umekauka. Umekauka nje lakini ndani ni mbichi Nitaukata*
*Ngariba: Wacheni kuogopa Kama wajinga wa milimani wasiojua kazi.*

Kutokana na wimbo huu, ngariba anaeleza kuhusu *mti uliokauka* nje lakini ndani ni *mbichi*. Hapa, mti uliokauka nje unaashiria hali ya kukomaa kwa watahiriwa. Kukomaa kwenyewe ni kwa kimaumbile, kiakili na kijamii kwamba wamehitimu kuvuka hadi katika kiwango cha utu uzima. Ngariba anaendelea kusema kwamba ataukata mti huo ambapo watahiriwa kupitia wimbo huo huo wanamruhusu kuukata. Hapa, mwimbaji anazilinganisha *mboo za watahiriwa* na *mti uliokomaa* au *kukauka* kijazanda. *Ubichi* unaorejelewa hapa ni ile hali ya mtahiriwa kuwa na uwezo wa kuzalisha, ambayo ni ishara ya kuiendeleza jamii. Kwa hivyo, mwimbaji anapitisha itikadi kuhusu tohara kwamba baada ya kupashwa tohara, mtahiriwa huwa amehitimu kuoa na kushiriki ngono ili kuiendeleza jamii. Kupitia kwa wimbo huu, watahiriwa wanahimizwa wasiwe na woga kama wale *wajinga wa milimani* wasiojua *kazi*. Maneno *wajinga wa milimani* yanarejelea Wakikuyu ambao wanaishi sehemu za milimani kinyume na Wakamba wanaoishi maeneo tambarare. Katika muktadha wa utamaduni wa Wakamba, watu wa milimani yaani Wakikuyu wanachukuliwa kuwa wavivu na ambao hawajiwezi kimapenzi (Wathome, 2009). Pamoja na hayo, neno *mbilano* (kazi) limetumika kjazanda kama ishara ya ngono. Hapa, watahiriwa wanashauriwa wawe jasiri kabla na hata baada ya tohara. Wanahimizwa wasiwe waoga katika masuala ya ngono kwenye ndoa kwa maana hiyo ndiyo njia ya pekee ya kupata watoto na hatimaye kuiendeleza jamii.

**Itikadi kuhusu Kazi**

Kazi ni shughuli anayoifanya mtu (TUKI, 2013). Shughuli yenyewe inaweza kuhusisha juhudi za kiakili na kimwili ili kufikia lengo fulani. Kazi ni sehemu muhimu ya maisha ya Wakamba na huchukua nafasi kubwa katika nyimbo zao za kiasili. Utafiti huu umetambua kwamba kupitia kwenye nyimbo za kiasili za Kikamba za kazi, itikadi kuhusu kazi hufumbatwa kijazanda na kujengwa kwa mielekeo mbalimbali. Kwa mfano, wimbo *Kaveti Kaanu* (Kijike Kizembe) unasimulia kuhusu mwanamke mzembe. Mwimbaji anamshauri kwamba hana budi kuchukua *kathungi* (chondo), *kamulo* (jembe) na *kavelu* (mbegu) na kisha aelekee shambani kufanya kazi ili aikimu familia yake. Angalia mishororo ifuatayo ya wimbo huu:

*Ndwose kathungi, kamulo na kavelu na uyaangiia muundani kaveti kaanu mbua ni mbiingu.*
*Syana iyamba kuvuna ii mbemba sya tumikeve twili.*
Tafsiri:
*Chukua chondo, jembe na mbegu na kisha uelekee shambani Kijike kizembe mvua imenyesha.*
*Watoto hawawezi shibishwa na mahindi ya serikali jamani mwaka mmoja mikebe miwili*

Kupitia wimbo huo huo, mwimbaji anapitisha itikadi kuhusu kazi kwamba ni muhimu kujitahidi kazini. Haya yanaelezwa vyema na Aju na wenzake (2013) wanaodai kuwa jamii nyingi za Kiafrika humthamini mtu anayefanya kazi na kuongeza kipato kinachosaidia kuendesha maisha yake, familia na jamii. Mwimbaji wa wimbo huu anaeleza kwamba mwanamke mvivu anafaa kuchangamka na kujitahidi kikazi *shambani* ili aweze kuikimu familia yake. Anaeleza kwamba chakula cha msaada wa serikali hakitoshi kuikimu familia kwa maana huwa kidogo mno. Hivyo, neno *tumikeve twili* (mikebe miwili midogo) ni jazanda inayorejelea *vyakula vya msaada* ambavyo haviwezi kutosha ikilinganishwa

na vile vinavyopatikana mtu anapowajibika kazini. Jazanda hii imetumika kuwasilisha itikadi ya umuhimu wa wanajamii kufanya kazi kwa bidii. Vilevile, maneno *chondo, jembe, mbegu* yametumika kijazanda kurejelea nyenzo muhimu za kazi. Kazi inayorejelewa hapa inaweza kuwa ya biashara, ofisi, sanaa na nyingineyo. Neno *muundani* (shambani) limetumika kijazanda kuashiria *maeneo ya kazi*. Jazanda hizi zote zimetumika katika kuifumbata itikadi inayohusiana na kazi kwamba kazi ni muhimu na kila mwanajamii hana budi kuwajibika ili kuchangia katika maendeleo ya jamii. Jazanda zenyewe zimetumika katika kukashifu na kukejeli uzembe miongoni mwa wanajamii.

Japo neno *Kaveti kaanu* (Kijike kizembe) limetumika kijazanda kuashiria mwanajamii yeyote mwenye uzembe, mwimbaji wa wimbo huu anamsawiri mwanamke kwa njia hasi inayoidunisha jinsia ya kike. Hivyo, matumizi ya "kijike" badala ya "mwanamke" yanaibua hali ya kumdunisha mhusika anayelengwa kwenye wimbo. Pamoja na hayo, wimbo wenyewe unapitisha itikadi ya kazi kwamba kazi za shambani zinafaa kushughulikiwa na wanawake. Mwelekeo unaowasilishwa hapa ni kwamba ni jukumu la mwanamke kushughulikia familia yake shambani ili wasihangaike kwa kukosa chakula. Hali hii inathibitisha maelezo ya Strobel (1979) kwamba kwa mujibu wa tamaduni nyingi za Kiafrika, mwanamke amepewa nafasi ya pili chini ya mwanamume katika mfumo wa kuumeni. Mwanaume anachukuliwa kuwa bora zaidi kuliko mwanamke. Hii ndiyo maana mwanamke analaumiwa zinapotokea changamoto kama vile njaa na kufeli kwa ndoa. Maoni ya mtafiti ni kwamba mume na mke hawana budi kuwajibika na kushughulika shambani pamoja ili kuikimu familia yao. Kazi za aina hii zinafaa kuwahusisha wazazi wote wawili. Tatizo kama vile la njaa linapotokea, mwanamke asiwe wa kulaumiwa peke yake kwa maana ndoa ni ya watu wawili na bila shaka ni sharti wote wawajibike.

**Itikadi kuhusu Ndoa na Mapenzi**

Kwa mujibu wa TUKI (2013), ndoa ni muungano kati ya mwanamume na mwanamke kuishi pamoja kama mume na mke hadi kifo kiwatenganishe. Akizungumzia dhana hii, Senkoro (1982) anaeleza kwamba asasi ya ndoa ni jambo muhimu na la lazima katika jamii. Wanajamii Wakamba huichukulia ndoa kuwa asasi muhimu katika maisha ya kila mwanajamii. Vijana walihimizwa kuoa au kuolewa baada ya kupashwa tohara. Kwenye hafla za ndoa na arusi, wanandoa husika huandaliwa mapochopocho pamoja na kuimbiwa nyimbo za aina mbalimbali kama ishara ya makaribisho katika familia ya bwana arusi. Nyimbo za kiasili za Kikamba zinaibainisha ndoa kama kiungo muhimu cha jamii. Kwa mfano, wimbo *Uka Usuvie Utwae* (Njoo Uitunze Ndoa) ni mojawapo wa nyimbo za kiasili za Kikamba zinazopitisha itikadi kuhusu ndoa. Tazama mishororo ifuatayo:

> *Niuiwe ngate, vamwe na kyavati ii, Niuiwe ngate, vamwe na kyavati ii kana ka mama uka usuvie utwae.*
>
> Tafsiri:
> *Umepikiwa mikate pamoja na chapati, umepikiwa mikate na chapati mtoto wa mama njoo utunze ndoa.*

Katika wimbo husika, mke mtarajiwa anaelezwa aje aitunze ndoa yake. Mwimbaji anawasilisha itikadi kuhusu ndoa kwamba mwanamke ana wajibu mkubwa wa kuitunza ndoa yake. Kwa kawaida, chapati na mikate ni miongoni mwa vyakula vinavyoandaliwa kwenye hafla mbalimbali katika jamii ya Wakamba. Maneno *ngate* (*mikate*) na *kyavati* (*chapati*) yametumika kijazanda kurejelea makaribisho makubwa katika jamii ya bwana arusi. Mwimbaji anawasilisha ujumbe kwamba binti huyu amekaribishwa katika ile jamii mpya na basi ni sharti awajibike katika kuitunza asasi hii muhimu. Maoni ya mtafiti ni kwamba utunzaji wa ndoa unawahusisha wanandoa wote wawili; mume na mke. Utunzaji wa ndoa usiegemee kwenye upande mmoja. Yaani, isiwe kwamba ndoa inapofeli mwanamke ndiye wa kulaumiwa.

**Itikadi kuhusu Ubikira**

Kwa mujibu wa TUKI (2013), ubikira ni hali ya kutomjua mwanamume au mwanamke kimwili. Katika jamii ya Wakamba, ubikira ulithaminiwa sana hasa kwa vijana wa kike. Vijana hawa walihimizwa kuutunza ujana wao hadi pale watakapohitimu kuwa mume na mke na kuanzisha ndoa. Kwa jamii ya Wakamba, ngono inafaa kuhifadhiwa kwa wanandoa pekee. Hivyo, wasichana waliopata mimba nje ya ndoa walidharauliwa. Itikadi kuhusu ubikira imepewa kipau mbele katika nyimbo za kiasili za Kikamba. Kwa mfano, itikadi hii inajitokeza katika wimbo *Sikala* ifuatavyo:

> *Manguleti nikwita ngikwita, ngwititye sikala ukambata na ung'endu*
> *Ngasokota yakwa na ngekia mwaki na ngainia uvuta.*
>
> Tafsiri:
> *Manguleti nakuita nakuita, nimekuomba sigara ukaninyima tu kwa ukaidi,*
> *Nikaikunja yangu na kuiwasha moto nikaanza kuivuta.*

Katika wimbo huu, mwimbaji amemwomba msichana Manguleti sigara bila mafanikio. Inaelezwa kwamba baada ya kunyimwa *sigara* alitafuta yake akaiwasha moto na kisha akaanza kuivuta. Neno *sigara* limetumika kijazanda kurejelea *ngono*. Pia, neno *mwaki* (moto) limetumika kuashiria hisia ya kutaka *kutoshelezwa kingono.* Wimbo *Sikala* umewasilishwa kijazanda kurejelea hali ya vijana wa kiume kutaka kuingiliana na wale wa kike kimapenzi. Tukio la Manguleti kumnyima mwenzake *sigara* limetumika kuwasilisha itikadi ya ubikira. Hapa, maarifa ya kimsingi yanatuwezesha kutambua kwamba kwa mujibu wa utamaduni wa jamii ya Wakamba, msichana hafai kujihusisha na ngono kabla ya kuolewa. Mwimbaji anawasilisha ujumbe kwamba ngono ni ya wale walio katika ndoa pekee. Hii ndiyo sababu inayomfanya mhusika wa kike Manguleti kumnyima mpenziwe wa kiume uhusiano wa aina hiyo. Mhimili wa nadharia ya Itikadi wa mielekeo unajitokeza katika wimbo huu. Jamii ya Wakamba ina mwelekeo kwamba ni marufuku kwa vijana wa kike kujihusisha na tendo la ndoa kabla ya ndoa. Hata hivyo, mtafiti anaonelea kwamba mwelekeo huu haujazingatia haki za kijinsia. Hii ni kwa sababu kijana wa kiume anaponyimwa sigara anatafuta nyingine anayoiwasha moto na kuanza kuivuta. Hali hii inaashiria namna ambavyo vijana wa kiume hufanya ngono bila kulaumiwa na wanajamii. Mtafiti anapendekeza kwamba suala la ubikira linafaa kuzingatiwa na vijana wote, wawe wa kike au kiume. Iwapo ubikira ni muhimu basi jinsia zote zihimizwe kuuzingatia.

**Itikadi kuhusu Utamaduni**

Utamaduni ni uzoefu wa kimaisha wa watu fulani (Wamitila, 2003). Kwa kawaida, neno hili huleta michakato ya kijamii ambayo huiwezesha jamii hiyo kujielezea na kujitambulisha pamoja na kufanya shughuli za kila siku. Hivyo, utamaduni unarejelea imani, tabia au ufahamu unaopokezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Kwa hivyo, utamaduni huhusisha vitu halisi, mawazo, thamani, mielekeo pamoja na mipangilio ya kitabia katika jamii husika. Utamaduni hupokezwa kupitia uzoefu wa jamii inayohusika. Uimbaji wa nyimbo za kiasili za Kikamba ni mojawapo wa uzoefu wa Wakamba. Utafiti huu umetambua kwamba nyimbo za kiasili za Kikamba husheheni mielekeo mbalimbali kuhusu itikadi za Wakamba, utamaduni ukiwemo. Kwa mfano, itikadi kuhusu utamaduni inajitokeza katika wimbo *Kithio kya Mukamba* (Utamaduni wa Mkamba).

Vol. 2 No. 2 (2024): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/jkal.v2i2.687


Angalia mishororo hii:

> *Kithio twatiie kyonze vyu kithio kitu*
> *Twai na mwathani mwathani wa ukamba Syokimau kithio tukituungiie*
> *Wamwithia Mombasa niwe Bakari niwe Juma Juma mukamba mwenda ndini syonze Mukamba ndusyoke syoka kithioni umanyiswe undu*
>
> Tafsiri:
> *Utamaduni tuliuacha wote kabisa utamaduni wetu*
> *Tulikuwa na nabii nabii wa Ukambani Syokimau tuurejeshe utamaduni.*
> *Ukimpata Mombasa ndiye Bakari, ndiye Juma, Juma Mkamba mpenda dini zote Mkamba si urudi rudi kwenye utamaduni ufundishwe jambo*

Katika wimbo huu, mwimbaji anaeleza namna ambavyo Wakamba wamekengeuka na kuzibugia dini za kigeni na kisha kuusahau utamaduni wao. Maneno *Bakari* na *Juma* ni majina ya Kiislamu yaliyotumika kijazanda kurejelea *ukengeushi* unaowakumba Wakamba. Jazanda hizi zimetumika kuupinga ukengeushi ili Wakamba waukumbatie na kuuonea fahari utamaduni wao. Kwa hivyo, wimbo huu unapitisha itikadi kuhusu utamaduni kwamba ni jambo muhimu linalofaa kuzingatiwa na Wakamba wasije wakawa watumwa wa tamaduni za kigeni. Mwimbaji anasisitiza kuwa majilio ya dini zingine hayamaanishi kuwa Wakamba wazitupilie mbali tamaduni zao. Maoni ya mtafiti ni kwamba uzoefu, tabia, vitendo na imani za kitamaduni zilizopitwa na wakati zinafaa kutupiliwa mbali. Hata hivyo, utamaduni unaofaa hauna budi kukuzwa, kuendelezwa na kuzingatiwa na wanajamii.

**Itikadi kuhusu Malezi**

Kulingana na TUKI (2013), malezi ni njia ya ukuzaji wa mtoto kwa kutarajiwa kufuata tabia na mwenendo unaostahiki. Hivyo, ni mbinu zinazohusishwa katika kuwalea na kuwakuza watoto kutoka kiwango kimoja hadi kingine maishani. Baloyi na wenzake (2019) wanaeleza kwamba katika utamaduni wa kijadi, ndoa huchukuliwa kuwa imekamilika inapokuwa na watoto na hasa wa kiume ambao huchukuliwa kama nguzo ya kijamii. Katika jamii ya Wakamba, inaaminika kuwa watoto ni mali ya jamii na kila mwanajamii ana wajibu wa kuwakuza na kuwalea. Malezi ya watoto hayana budi kuzingatia tamaduni na maadili ya Wakamba. Itikadi kuhusu malezi imewasilishwa kupitia wimbo *Kyathi no Vala* (Miadi ni ileile). Angalia sehemu hii:

> *Iyaii yayai! kyathi no vala vala wandavisye wambiie ninguka kuathima mwana ii na kaindo ngyuka.*
>
> Tafsiri:
> *Iyaaiii, aiii! miadi ni ile ile, vile ulivyoniambia uliniambia utakuja kumbariki mtoto na kijitu ukija.*

Katika wimbo *Kyathi no Vala* (Miadi ni ileile) mwimbaji anaanza kwa kueleza kwamba alikuwa ameahidi kuwa angekuja kumbariki mtoto na *kijitu*, yaani kitu kidogo. Kwenye jamii ya Wakamba, kuzaliwa kwa mtoto huwa ni ishara ya kuendelea kwa jamii hiyo kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Mtoto anapozaliwa jamii husherehekea na kumzawadi mama pamoja na mtoto aliyezaliwa, kama ishara ya kuwajibika kijamii kuhusiana na malezi ya mtoto anayehusika. Neno *kaindo* (kijitu) ni jazanda inayorejelea zawadi yoyote kwa mtoto anayesherehekewa kuzaliwa kwake. Itikadi inayowasilishwa hapa inahusu malezi kwamba watoto ni wa jamii na kila mwanajamii ana jukumu la kuwalea watoto hao.

Vilevile, tukio la wanajamii la kumtembelea mama na mtoto linaashiria upendo na mapenzi yao kwa mtoto ambaye ndiye mwanajamii mgeni. Tukio hili ni njia mojawapo ya kumkaribisha mtoto anayehusika katika jamii. Akizungumzia hoja hii, Boss (1998) anaeleza kwamba watoto hujifunza kupenda na kupendwa katika familia walimozaliwa. Kwa hivyo, Wakamba wanaamini ni vigumu kwa mtu ambaye hakupata kupendwa utotoni mwake kuonyesha upendo kwa wengine.

**Itikadi kuhusu Mauti**

Mauti ni kifo au hali ya kiumbe kukosa uhai (TUKI, 2013). Itikadi kuhusu mauti inahusu imani, mielekeo na mawazo ya wanajamii kuhusiana na mauti. Utafiti huu umetambua kwamba nyimbo za kiasili za Kikamba huwasilisha itikadi kuhusu mauti. Mfano ni kama vile wimbo *Kikw'u ni Musyimi* (Kifo ni Mwindaji). Tazama mishororo ifuatayo ya wimbo huu:

*Kikwu ni musyimi ute tei.*
*Ni muvutani ute tei.*
*Okaa kwosa kila kiseo na kutia mwene na kimeto kitathimika.*

**Tafsiri:**
**Kifo ni Mwindaji**
*Kifo ni mwindaji asiye huruma.*
*Ni mnyang'anyi asiye na huruma.*
*Huja kuchukua kile chema na kumwacha mwenyewe na huzuni isiyopimika.*

Mielekeo ni mojawapo wa mihimili ya nadharia ya itikadi. Kupitia wimbo huu tunapata mielekeo mbalimbali inayoijenga itikadi ya mauti katika jamii ya Wakamba. Kwanza kabisa, mauti inachukuliwa kama namna ya unyang'anyi au wizi. Maneno *Musyimi ute tei* (Mwindaji asiye na huruma) na *Muvutani ute tei* (Mwizi asiye na huruma) yametumika kijazanda kurejelea kifo ambapo kinalinganishwa na mnyang'anyi na mwizi asiyekuwa na huruma. Jazanda hizi zinawasilisha uchungu wanaohisi wafiwa baada ya kuachwa na mpendwa wao.

Katika jamii ya Wakamba, mauti huwa miongoni mwa mambo mazito wanayokabiliana nayo katika safari ya maisha yao. Hata hivyo, Wakamba huamini kwamba mauti sio mwisho wa maisha kwani wao hushikilia imani kwamba kuna wakati watakapokutana na wale waliowatangulia kwenye ulimwengu mwingine. Hivyo, imani hii ndiyo huwapa wafiwa faraja kwa kujua kwamba huo sio mwisho wao wa kupatana na wapendwa wao.

**Hitimisho**

Makala haya yameshughulikia uhakiki wa itikadi zilizofumbatwa kijazanda kwenye nyimbo za kiasili za Kikamba. Utafiti wenyewe umegundua kwamba waimbaji wa nyimbo za kiasili za Kikamba hufumbata itikadi za Wakamba kijazanda kwenye nyimbo husika. Itikadi hizo ni kama vile umuhimu wa kupashwa tohara, umuhimu wa kujitahidi kazini, umuhimu wa ndoa na mapenzi, umuhimu wa ubikira miongoni mwa vijana, umuhimu wa utamaduni, namna ya malezi pamoja na umuhimu wa mauti miongoni mwa wanajamii.

**Marejeleo**

Aju, O. & Ilamosi, E. (2013). The Meaning of Work from the Nigerian Perspective. *European Journal of Business and Management, 5(22), 154*-162.

Althusser, L. (1984). *Essays on Ideology*. Verso Publications.

Baloyi, M. E., & Manala, M. J. (2019). 'Reflections on challenges of preferring the male child in an African marriage. A practical theological observation. *Verbum et Ecclesia 40(1),* a1852. https://doi.org/10.4102/ve.v40i1.1852

Boss, P. (1998). *Family Stress Management.* Sage Publications.

Eagleton, T. (2007). *Ideology: An introduction*. Verso Publications.
Gianetti, L. (2013). *Understanding Movies Ideology*. Pearson Publisher.
Gramsci, A. (1985). *Selections from Cultural Writings.* Lawrence and Wishart.
Khan, N. (2021). Relationship between Literature and Life. *Scholars Journal of Arts, Humanities and Social Sciences.* Abbreviated Key Title: Sch J Arts Humanit Soc Sci ISSN 2347-9493 (Print) | ISSN 2347-5374 (Online) Journal homepage: https://saspublishers.com
Lakoff, G. & Johnson, M. (1993). *The contemporary theory of metaphor.* Katika https://escholarship.org/uc/item/54g7j6zh
Mohamed, S. A. (1995). *Kunga za Nathari ya Kiswahili: Tamthilia, Riwaya na Hadithi Fupi.* E. A. E. P
Senkoro, F. E. M. K. (1982). *Fasihi*. Press and Publicity Centre.
Strobel, M. (1979). *Muslim Women in Mombasa; 1890-1975.* Yale University Press.
TUKI. (2013). *Kamusi ya Kiswahili sanifu*. Oxford University Press.
Van Dijk, T.A. (1998). *Ideology: A Multidisciplinary Approach*. SAGE Publications.
Vincent, A. (1992). *Modern Political Ideologies*. Blackwell.
Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi. Istilahi na Nadharia.* Focus Publishers.
Wathome, R. (2009). *Mtindo Katika Nyimbo za jamii ya Wakamba wa Masaku ya Kati* (M. A. Thesis, Kenyatta University).